



Mchoro wangu



Tusome Early Literacy Programme


Mchoro wangu



Jina langu ni Ali na hili ni darasa langu.
Ninalipenda darasa langu.

Mwalimu wangu ni Bibi Halima.

Bibi Halima amesimama darasani karibu na ubao.




Bibi Halima anawatazama watoto wakichora michoro wakiwa wamekaa kwenye dawati. Mimi nimechora mchoro wangu katika kitabu nikitumia penseli.



Bibi Halima amesema mchoro wangu ni mzuri.

Bibi Halima amesema ni saa ya kwenda nyumbani.







Nimeupeleka mchoro wangu nyumbani.
Mama amefurahi kuuona mchoro wangu.


Mchoro huo ni wa darasa langu.

Mama amesema mchoro wa darasa langu ni mzuri.





Mchoro wangu una rangi za kupendeza.
Mchoro wangu una ubao, dawati na vitabu.



Pia una kabati, kichongeo na kifutio.

Watoto wote darasani walivutiwa na mchoro wangu.

Maswali

1. Mwalimu wa Ali anaitwa nani?
2. Wanafunzi wameketi wapi?
3. Ali amechora mchoro akitumia nini?
4. Mchoro wa Ali ni wa nini?
5. Taja vitu vilivyo katika mchoro wa Ali.

Mchoro wangu

Ali yuko darasa la kwanza. Mwalimu wao, Bi. Halima anawapatia kazi ya kuchora. Je, Ali alichora mchoro wa nini?



Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.